



JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA

HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA MAWENZI



AFYA KILIMANJARO
Simu Na Moshi 027 52321
E-mail: barua@mawenzirrh.go.tz
(Barua zote ziadikwe kwa
Mganga Mfawidhi wa Hospitali)

S. L. P. 3054,
MOSHI.

09/4/2026

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MKATABA

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mawenzi ni taasisi ya afya ya umma inayotoa huduma za matibabu, kinga na elimu ya afya kwa jamii. Hospitali inalenga kuboresha utoaji wa huduma kwa kuajiri watumishi wa mkataba ili kuziba mapungufu ya rasilimali watu katika kada mbalimbali.

Hivyo, hospitali inakaribisha maombi kutoka kwa Watanzania wenye sifa stahiki kujaza nafasi zifuatazo:

1. DAKTARI DARAJA LA II (Nafasi 1)

Majukumu:

- Kutoa huduma za matibabu kwa wagonjwa wa nje na wa ndani
- Kufanya uchunguzi na kutoa tiba sahihi
- Kusimamia wagonjwa waliolazwa wadini
- Kushiriki katika shughuli za dharura na upasuaji inapohitajika
- Kutoa elimu ya afya kwa wagonjwa

Sifa:

- Shahada ya Udaktari (MD au sawa)
- Usajili na leseni hai kutoka Baraza husika

2. DOBI DARAJA LA II – (Nafasi 2)

Majukumu:

1. Kukusanya nguo chafu
2. Kufua nguo
3. Kukausha na kupiga pasi
4. Kuhifadhi nguo safi
5. Kusambaza nguo safi
6. Kutunza vifaa vya kufulia
7. Kuzingatia usalama na afya kazini
8. Kutunza kumbukumbu
9. Kushirikiana na timu ya afya

Sifa:

- Elimu ya kidato cha nne au zaidi
- Mafunzo ya msingi ya afya

3. AFISA USTAWI WA JAMII MSAIDIZI DARAJA LA II (Nafasi 1)

Majukumu:

- Kutoa ushauri wa kijamii kwa wagonjwa na ndugu zao
- Kufuatilia kesi za kijamii (watoto, wazee, waathirika)
- Kuratibu huduma za msaada wa kijamii
- Kushirikiana na wadau wa kijamii

Sifa:

- Cheti au Diploma ya Ustawi wa Jamii

4. MSAIDIZI WA HESABU DARAJA LA II (Nafasi 14)

Majukumu:

- Kuandaa na kusimamia kumbukumbu za kifedha
- Kukusanya na kurekodi mapato ya hospitali
- Kuandaa taarifa za fedha
- Kusimamia malipo na matumizi ya fedha
- Kuhakikisha uzingatiaji wa taratibu za fedha

Sifa:

- Diploma au Shahada ya Uhasibu/Fedha

5. MHUDUMU WA AFYA (HEALTH ATTENDANT) – (Nafasi 3)

Majukumu:

- Kusaidia wagonjwa katika mahitaji ya msingi
- Kusafisha na kuandaa mazingira ya hospitali
- Kusafirisha wagonjwa na vifaa
- Kusaidia wauguzi katika kazi za kawaida

Sifa:

- Elimu ya kidato cha nne au zaidi

6. AFISA HUDUMA KWA WATEJA (CUSTOMER CARE) – (Nafasi 5)

Majukumu:

- Kupokea na kuelekeza wagonjwa
- Kushughulikia malalamiko na maoni ya wateja
- Kutoa taarifa sahihi za huduma za hospitali
- Kuhakikisha wateja wanapata huduma kwa wakati

Sifa:

- Diploma/Shahada katika uhusiano wa umma au biashara

7. AFISA HABARI DARAJA LA II (Nafasi 1)

Majukumu:

- Kusimamia mawasiliano ya hospitali
- Kuandaa taarifa kwa vyombo vya habari
- Kusimamia mitandao ya kijamii ya taasisi
- Kuratibu kampeni za elimu ya afya

Sifa:

- Shahada ya Mawasiliano ya Umma/Uandishi wa Habari
- Uzoefu katika kupiga picha, kurekodi, kupanga na kuhariri video,
- Uzoefu wa kutengeneza michoro (graphic design)

8. AFISA MUUGUZI MSAIDIZI DARAJA LA II (Nafasi 6)

Majukumu:

- Kutoa huduma za uuguzi kwa wagonjwa
- Kusimamia utoaji wa dawa na huduma za kliniki
- Kufuatilia hali ya wagonjwa
- Kushirikiana na madaktari katika matibabu

Sifa:

- Cheti au Diploma ya Uuguzi
- Usajili na leseni hai

9. AFISA TEHAMA DARAJA LA II (Nafasi 3)

Majukumu:

- Kusimamia mifumo ya TEHAMA ya hospitali
- Kutunza na kurekebisha vifaa vya kompyuta na mtandao
- Kusimamia mifumo ya taarifa za wagonjwa (Hospital Systems)
- Kutoa msaada wa kiufundi kwa watumishi
- Kuhakikisha usalama wa taarifa (data security)

Sifa:

- Diploma au Shahada ya TEHAMA/Computer Science
- Uzoefu wa mifumo ya hospitali utapewa kipaumbele

10. MHUDUMU CHUMBA CHA KUHIFADHI MAITI (Nafasi 4)

Majukumu:

- i. Kupokea na kuhifadhi miili ya marehemu
- ii. Kufanya usafi na kuandaa mwili
- iii. Kusaidia taratibu za uchunguzi (Postmortem)
- iv. Kusimamia utunzaji wa kumbukumbu
- v. Kukabidhi miili kwa ndugu
- vi. Kufanya usafi wa mazingira ya kazi
- vii. Kusimamia udhibiti wa maambukizi
- viii. Kusimamia utunzaji wa vifaa

Sifa:

- Elimu ya kidato cha nne au zaidi
- Mafunzo ya msingi ya afya au mortuary

MASHARTI YA JUMLA

- Awe raia wa Tanzania
- Awe na nidhamu, uadilifu na kujituma
- Awe tayari kufanya kazi kwa mkataba

JINSI YA KUOMBA

Waombaji watume:

- Barua ya maombi
- CV
- Nakala za vyeti
- Mawasiliano ya wadhamini wawili

Kwa:

Mganga Mfawidhi

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mawenzi

S.L.P 3054

Moshi, Kilimanjaro

Au barua pepe: barua@mawenzirrh.go.tz

MWISHO WA MAOMBI: TAREHE 17/04/2026

Kumbuka: Waombaji watakaokidhi vigezo pekee ndio watakaoitwa kwenye usaili.

Imetolewa na;


Dkt. Abilah Issa
MGANGA MFAWIDHI
HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA MAWENZI
S.L.P. 3054 MOSHI

HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA MAWENZI